Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Enyi mlioamini, si halali kwenu kuwarithi wanawake kwa nguvu; wala msiwazuie (kuolewa) ili mpate kuwanyang'anya baadhi ya vile mlivyowapa, isipokuwa wawe wamefanya uovu ulio wazi; na kaeni nao kwa wema ; na kama mkiwachukia, basi huenda mchukie kitu na AllahAmetia heri nyingi ndani yake. (An-Nisaa 4:20)

JUZU 82 No. 239 | AKHIRA - RAJAB. 1444 AH | JANUARI. 2023 AD | ZAHOOR 1402 HS | BEI TSH. 700/=

Ahmadiyya yakutana na viongozi wakuu wa Nchi

Na.
Mahmood Hamsin Mubiru
(Kiwalani, Dar es Salaam)

2022 kwa Mapenzi na huruma ya Allah ni mwaka ambao, umeacha alama ya kudumu kwenye mchango wa Hisitoria ya Ahmadiyya Tanzania kutokana na juhudi kubwa iliyofanywa na viongozi wa Jamaat katika kufikisha ujumbe wa Islamu kwa viongozi wakuu wa Nchi, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Makamu wa Raisi Dr. Isidore Mpango, Spika wa Bunge la Tanzania Dr. Tulia Ackson na Raisi wa Tanzania Dr. Samia Suhulu Hassan.



Picha ya pamoja ya Raisi wa Tanzania na wawakilishi wa Jumuiya ya Ahmadiyya siku ya matembezi. Wa kwanza kulia akiwa ni Sadr Lajna Bi. Zena Nyange, wa pili Katibu Yahaya Y. Kambaulaya, wa tatu Naibu Amir Abid M. Bhatti, wa nne ni Raisi wa Tanzania Mh. Dr. Samia S. Hassan, wa tano Amir Sahib Sh. Tahir M. Chaudhry, wa sita Naibu Amir Sh. Abdul-Rahman M. Ame na wa saba ni Katibu Mkuu Seif H. Nakuchima.

Uongozi wa Jamaat kwa hakika unafuata nyayo za Mtukufu Mtume Muhammad[saw] ambaye aliwaandikia viongozi na wafalme wa enzi hizo ili wapokee ujumbe wa Islamu na hatimae wajiunge na Islam. Hisitoria inatukumbusha kuwa aliwaandikia Mfalme wa Roma Heraclius, Mfalme wa Iran, Mfalme Negus wa Abyssinia, Muqaugis wa Misri – kuwataja wachache. Utamaduni huo umeendelezwa na mwanae wa kiroho Hazrat Mirza Ghulam Ahmad[as] Masih na Mahd, ambaye alimwandikia Malkia Victoria vitabu viwili kumueleza kuwa yeye ndie Masih na nusura ya Ufalme wake. Itatokana na kujiunga na Islam. Vitabu viwili navyo ni:- ***Sitara-e-Qaisarab*** na ***Tohfa-e-Qarsariyyah***, ambavyo vyote vinaeleza ubora wa Islamu. Katika ***Sitara-e-Qaisarab*** anapinga ujaji wa Masih mwenye kutumia upanga, katika kueneza mafundisho yake na kuwalazimisha watu kuingia katika Islam. Amefutilia mbali dhana potofu ya Jihadi na kusisitiza kuwa katu Islam haikuenezwa kwa Upanga. Kafara ya Yesu haiingii akilini na maelezo yakina kuhusu madai yake ya kuwa Masih Aliyeahidiwa. Katika ***Tohfa-e-Qarsariyyah*** anaendelea kueleza uzuri wa Islam, ambayo pekee ndiyo inaweza kudumisha amani na udugu Duniani. Ukweli wa Mtukufu Mtume Muhammad[saw] na Islam kwa ujumla. Alimtaka Malkia aitishe mkutano wa Dini zote, ili kila Dini ieleze mafundisho yake.

Endelea uk. 5

Ijtima'a ya Majlis Ansarullah 2022

Na.
Ally Hamisi Mbambwa
Sadr Majlis Ansarullah - Tanzania

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ

Majlis Ansarullah Ahmadiyya -Tanzania ilifanya Ijtimaa pamoja na Majlis Shura ya kitaifa tarehe 09 hadi 11, December, 2022.

Baada ya sala ya Ijumaa iliyoongozwa na Maulana sheikh Abdulrahman Ame sahib, Ijtima'a ilianza rasmi kwa Upandishaji bendera majira ya saa tisa Alasiri, ambapo Sadr majlis Ansarullah Bw. Ally Hamisi Mbambwa Alipandisha bendera ya Tandhim na Naib Amir Tabligh na Tarbiyyat Sheikh Abdulrahman Ame sahib, alipandisha bendera ya Serikali.

Baada ya ufunguzi wa Ijtimaa kwa usomaji wa Quran Tukufu, ilifuata kiapo cha Majlis Ansarullah na hotuba ya ufunguzi iliyotolewa na Sadr Majlis Ansarullah . kauli mbiu ya Ijtima'a yam waka huu ilikuwa ni **"Qur an Tukufu"**, hivyo katika hotuba yake, Sadr Sahib aliwakumbusha Ansarullah kutekeleza agizo la Khalifa mtukufu wa tatu Mirza Nasir Ahmad rh.i kwamba kila mmoja wao anapaswa kusoma na kuhifadhi aya 17 za mwanzo katika suratil Baqara zinazoelezea makundi ya aina tatu. Kundi la waaminio, kundi la makafiri na kundi la wanafiki. Hivyo akawahimiza kufuata na kutekeleza sifa zote za kundi la waaminio kwani ndilo kundi lenye salama.



Amir na Mbashiri alipata picha ya pamoja na Sadr Majlis Ansarullah Tanzania pamoja na wajumbe wote wa Tanzeem, mara baada ya kufunga Ijtimaa hiyo siku ya Tarehe 11 . Disemba 2022

Kisha washiriki wote walisikiliza Hotuba ya sala ya Ijumaa mbashara iliyotolewa na Khalifa Mtukufu wa tano kupitia MTA.

Katika ijtimaa yetu kulikuwa na Majlis shura, mwaka huu tulikuwa na Ajenda tatu. Ajenda ya uchaguzi wa sadr majlis na Naib Sadr saf Dom. Na ajenda ya pili ilikuwa ni bajeti ya mwaka 2023 na ajenda ya jengo la ofisi za Ansarullah. Uchaguzi ulifanyika kwa ufanisi na msimizi wa uchaguzi alikuwa ni Amir na Mbashiri mkuu Sheikh Tahir Mahmood Choudhry sahib.

Katika Ijtimaa kulikuwa na mashindano mbalimbali ya kielimu na ya kimwili. Katika mashindano ya kielimu kulikuwa na usomaji wa Qur an Tukuf tafsiri, Hifdh na tilawat. Hadith za Mtume[saw], utoaji wa Hotuba, kuhifadhi na kughani mashairi, chemsha bongo n.k.

Na katika mshindano ya kimwili kulikuwa na michezo ya mpira wa miguu, riadha, nguvu za mikono, kulenga shabaha, kukalia kiti, kufikisha taarifa, Draft, bao na mingineyo.

washindi walikabidhiwa zawadi na Amir na Mbashiri Mkuu Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry sahib wakati akifunga Ijtimaa hiyo siku ya Jumapili jioni.

Mapema kabla ya ufungaji wa Ijtima'a, mgeni rasmi Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya waislam wa

Endelea uk. 7

Amri ya utii wa Nidhamu ya Jamaat Uk. 3

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Hisabani Yasira

Mfanyabiashara mahiri anasifa kuu mbili nzuri. Kwanza anamaizi kuwa ***Mali bila Daftari hupotea bila Habari***. Na la pili kila jioni bila kukosa kukagua mwenendo wake wa tijara iwapo amepata faida au hasara. Tathmini ya kila siku inampa fursa ya kujirekebisha na kuweka mambo sawa. Kwani siku zote anakumbuka ***usipoziba ufa utajenga ukuta***.

Mwaminio ni Mfanyabiashara mkubwa na ana Bahati kubwa kuwa yeye anafanya Biashara na Allah. Sehemu kadhaa za Kurani Tukufu. Mwaminio ameambiwa faida ya kufanyabiashara na Allah. Biashara hii ni kutekeleza Amri zote za Allah zinazopatikana katika Kuruani Tukufu, amri ambazo zimetekelezwa na Mtukufu Mtume Muhammad[saw] na zama hizi kutekelezwa kwa vitendo na mwanae wa Kiroho, Masih aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as].

Jioni kila siku ni muhimu ukae chini utafakari ni kwa njia gani umepitisha siku yako. Ni Makosa mangapi umeyatenda. Ni wema upi ulioufanya? Je umefanikiwa Kusoma Kuruani Tukufu? Hadith za Mtukufu Mtume[saw]? Vitabu vya Masihi aliyeahidiwa ambavyo kwa msaada wa Allah wataalamu wetu wamevitafsiri katika lugha yetu adhimu ya Kiswahili? na Je umetafakari kuhusu hayo uliyoyasoma? Mara ngapi kwa Siku umemsalia Mtukufu Mtume Muhammad[saw]? Umempa Faraja Mgonjwa? Miba uliyokuta njiani umeitoa? Umeipunguza njaa kwa yule ambaye hajaweka Riziki Tumboni? Mtumishi wako umekaa nae Meza moja kula chakula pamoja? Lile Deni lako umelilipa au umelipunguza? Umekwenda kuomba msamaha kwa yule aliyekukosea wewe? Hiyo nguo uliyovaa umemshukuru Allah? Umekwenda Msikitini na kuzingatia kanuni zote zinazotakiwa kuzingatiwa? Umekubali siku ipite bila kutizama MTA ili ujiimarishe Kiimani? Umeiombea Nchi yako ipate maendeleo ya kweli? na hatimae kumpokea Masih aliyeahidiwa?

Hayo na mengine mengi unatakiwa uyafanyie Tathmin kila siku kwani hakuna Binadamu ajuaye siku ya kuondoka. Inabidi ukumbuke kuwa wazo zima la kufanya tathmini ya kila siku lilitolewa na Kiongozi wetu Mpendwa Khalifatul Masih wa (V) Hadhrat Mirza Masroor Ahmad[atba] katika ziara yake ya hivi karibuni nchini Marekani.

Agizo linalotoka kwa Huzur linatakiwa litekelezwe kwa Mapenzi na Jazba kubwa. Bila shaka siku zetu hizi kazi ya Biashara ya kiroho ni ngumu. Kuna siku unapata Faida na kuna siku unapata Hasara. Ufaulu wako utakuwa ni kumkabidhi Allah maisha yako. Ujitahidi kumuomba Allah kwa kudumu na kwa Imani ili kila nukta ya Maisha yako hapa Duniani iwe ya Kupata radhi ya Allah. Na huo ndio ufaulu Mkuu. Tunamshukuru "Allah kwa neema zote alizotuneemesha katika Mwaka 2022 na kwa unyenyekevu mkubwa tunaomba yale yote utakayoridhia kwa ajili yetu katika Mwaka 2023".



QUR'AN TUKUFU

وَالشَّمْسِ وَضُحَاهَا — Naapa kwa jua na mwanga wake!

وَالْقَمَرِ إِذَا تَلَاهَا — Na kwa mwezi unapoliandama!

وَالنَّهَارِ إِذَا جَلَّاهَا — Na kwa mchana unapolidhihirisha!

وَاللَّيْلِ إِذَا يَغْشَاهَا — Na kwa usiku unapolifunika! (Sura Ash-Shams.1-4)

NUKUU YA HADITHI

HADITH

عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ، قَالَ: سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ، يَقُولُ: لَا تَقُومُ السَّاعَةُ حَتَّى تَطْلُعَ الشَّمْسُ مِنْ مَغْرِبِهَا، فَإِذَا طَلَعَتْ وَرَآهَا النَّاسُ آمَنَ مَنْ عَلَيْهَا، فَذَلِكَ حِينَ لَا يَنْفَعُ نَفْسًا إِيمَانُهَا لَمْ تَكُنْ آمَنَتْ مِنْ قَبْلُ.(ابن ماجہ۔ كتاب الفتن.باب ظلوع الشمس من مغربها.نمبر۔۴۰۶۸).

Hazrat Abu Huraira[ra] anasimulia kuwa yeye alimsikia Mtume[saw] akisema: Kiyama haitasimama mpaka jua lichomoke upande wa maagharibi na litakapochomoka na watu wataliona, wataamini wote ilhali haitafaa kwa nafsi yeyote Imani yake isiyoamini kabla yake.

Hazrat Ahmad[as] anasema: Hatimaye Tauhiid (umoja wa Mungu) itashinda. Miungu mingine itaangamia na mwabudiwa wa uwongo watatenganishwa na Uungu wao…. Itakuwepo ardhi mpya na mbingu mpya. Sasa zinakaribia siku ambamo jua la ukweli litachomoka kutoka kwa upande wa Magharibi na Ulaya itapata kujua juu ya Mungu wa kweli na baada yake mlango wa tauba utafungwa kwani wenye kuingia humo wataingia kwa nguvu kubwa na watabakia wale tu ambao wamefungiwa milango kwa tabia nao wanalipenda giza si nuru. Hivi karibuni mila zote zitaangamia isipokuwa Islam na mila zote zitaharibika ila mila ya kimbingu ya Islam ambayo haitapinda wala kukatika, hadi kuuvunja udajjali. Wakati unakaribia ambamo umoja wa kweli wa Mungu utaenea kwenye kila nchi ambayo wanauhisi mioyoni mwao wakazi wa jangwani na wale walioghafilika na mafundisho yote. Siku hiyo haitabakia(haitakuwepo) kafara ya bandia wala mungu yoyote wa bandia."**(مجموعہ اشتہارات جلد ۲ ۳۰۵.۳۰۴)**

سنو اب وقتِ توحیدِاتم ہے۔ ستم اب مائل مُلکِ عدم ہے
خدا نے روک ظلمت کی اٹھادی۔فسبحان الّذی اخزی الاعادی

Tafsiri: Sikilizeni! Muda huu ni wa Umoja kamili.
Zindukeni! Jeuri unaelekea kuisha. Mwenyezi Mungu Amekwisha ondoa vikwazo vya giza basi utukufu ni wa Yule Aliyewafedhehesha maadui.

UJUMBE WA KHALIFA MTUKUFU KUHUSU MWAKA MPYA

Khalifa Mtukufu (atba) Aliwahutubia wanajumuiya duniani kote kwa hotuba yake ya Ijumaa iliyotolewa tarehe 31-12-2021 kutoka Masjid Mubarak U.K. na mwishoni mwa hotuba yake alisema kuwa mwaka mpya unaanza kesho na Aliomba, Mwenyezi Mungu aufanye mwaka huu mpya kuwa wenye baraka kwa Jumuiya na wanajumuiya wote. Jumuiya ihifadhiwe na maovu yote, na njama zote dhidi ya Jumuiya hii zisifanikiwe. Na tuwe miongoni mwa wanaoshuhudia utimilifu wa ahadi aliyoitoa Mwenyezi Mungu kwa Masihi Aliyeahidiwa (as).

Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba tunapaswa kuingia katika mwaka mpya kwa maombi. Tahajjud inapaswa kuswaliwa,na misikiti mingi inapanga kwa ajili ya hili. Wale ambao bado hawajapanga mipango wafanye hivyo. Ikiwa haiwezekani kusali katika jamaa, basi watu wanapaswa kusali Tahajjud mmoja mmoja majumbani mwao na waendelee kufanye maombi mengi na wajijengee na tabia ya namna hii kwa siku zote.

Khalifa Mtukufu (atba) alisema kuwa pamoja na Durood Sharif [sala juu ya Mtume (saw)] na Istighfar [kuomba msamaha], dua zifuatazo zapaswa kusomwa:

"Mola wetu, Usiipotoshe mioyo yetu baada ya kutuongoza, na Utupe rehema kutoka Kwako, hakika Wewe ndiwe Mpaji Mkuu. (3:9)

"Mola wetu, Tughofirie madhambi yetu na kupita kwetu kiasi katika mambo yetu na uiimarishe miguu yetu na Utusaidie juu ya watu makafiri." (3:148) .

Tunawatakiwa wasomaji wetu wote wanaopatikana duniani kote, heri nyingi na baraka tele za mwaka mpya 2023. Aamin.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe: 1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Amri ya utii wa Nidhamu ya Jamaat



Sheikh Abdul-Rahman Muhammad Ame Sahib

Kujitolea Kifedha katika nji ya Allah.

Aya juu ya utii

Hizi ni aya chache miongoni mwa nyingi katika Quran tukufu zikiwapatia waaminio amri na maagizo ya namna ya kuwa watiifu kwa Mwenyezi Mungu, Mtume Wake na viongozi wao pamoja na kueleza kwamba waaminio wakweli daima huwa na kauli hii tu ya ***Samiina wa atwanaa.***

Katika Hadithi iliyosimuliwa na Hadhrat Abu Huraira juu ya utii kwa wenye madaraka, Mtukufu Mtume s.a.w. amesema:

Ni juu yako kusikia na kutii katika dhiki yako na faraja yako, na katika furaha yako na karaha yako na hata kama mwingine amependelewa dhidi yako (Muslim).

Maneno ya Masihi Aliyeahidiwa na Makhalifa juu ya utii:

Utii ni jambo la aina hii kwamba kama utatekelezwa kwa moyo wa kweli, basi moyoni huja nuru fulani na rohoni huja ladha fulani na mwanga. Jitihada za ibada huwa hazihitajiki kwa kiwango kile kinachohitajika katika utii, lakini kuna sharti hili kwamba utii huo uwe wa kweli na hili ndilo jambo lililo gumu. Katika utii ni lazima kuzichinja tamaa zako za nafsi, bila ya hivyo utii hauwezi asilan kuwepo. Na matamanio ya nafsi ni kitu cha aina hii ambacho kinaweza kuwa sanamu hata ndani ya mioyo ya wacha Mungu wakubwa, wakati mwingine hata wale wenye kudai kuzama sana ndani ya umoja wa Mwenyezi Mungu nao pia hutoka nje ya utii. Hutengeneza sanamu (za matamanio ya nafsi zao).

Alisema zaidi: Hakuna kaumu yoyote iwezayo kusemwa kuwa ni kaumu wala haipulizwi humo roho ya umoja na ushirikiano, hadi itakapotekeleza kanuni za utii. Acheni kuhitilafiana katika rai na mtiini yule ambaye Allah Ameagiza atiiwe. Kisha kazi ile aitakayo hufanyika. Mkono wa Allah uko pamoja na Jumuiya. Hii ndio siri iliyomo ndani yake. Allah huipenda Tauhidi (Umoja Wake) na umoja huu hauwezi kustawi kama utii hautakuwepo«.)Tafsir Hadhrat Masihul Mauud a.s. jal. 2 uk 246-247, Tafsir Suratun Nisaa:59, Alhakam jal. 5 No. 5 tarehe 10 Februari 1901.(

Hadhrat Khalifatul Masih Awwal r.a. aliwahi kusema juu ya utii kwamba" :Jiweke mikononi mwa lmamu kama muosha maiti. Kama vile ambavyo mfu hawezi kujigeuza wala kufanya chochote na mwenye kumuosha ndio humgeuza geuza,vivyo hivyo ni lazima kwa mwenye kutii kikamilifu kwamba ajikabidhi kwenye mikono ya Imam, na kiwango hiki kitakapo kuwepo ndipo tutaweza kuwa wenye kuitekeleza ahadi ya Baiat. Ndipo tutakapokuwa wenye uwezo wa kupata viwango vile vya utii vilivyosemwa na Allah na Mtume wake.

Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad r.a. alikuwa akisema kwamba mimi hushikilia rai yangu katika baadhi ya masuala na huziweka rai zangu binafsi kwa Khalifatul Masih kwa dalili, lakini kama rai yangu ikataliwe basi huwa haijawahi kunijia wazo kwamba kwa nini rai yangu imekataliwa au rai yangu ilikuwa ni nini. Kisha rai ya Khalifa wa zama huwa ndio inakuwa rai yangu .Kisha huitekeleza amri hiyo iliyotolewa na Khalifa wa zama, kwa utii kamili.

Hadhrat Khalifatul Masih V

Mwislamu wa kiahmadiyya anapswa kuona hivi kwamba, Islam imewapa waumini wake kila aina ya uhuru unaojuzu na uhuru uliomo ndani ya Islamu sidhani kama wapatikana ndani ya dini zingine, bali kinyume chake hamna. Lakini baadhi ya mipaka imeyowekwa ni kwa ajili ya kuzirekebisha khulka zake mwenyewe na kwa ajili ya maendeleo ya kiroho na kwa ajili ya kustawisha umoja wa Jumuiya na ni muhimu kubakia ndani ya mipaka yake .*Hotuba ya Ijumaa 6 June 2014.*

Maana ya Utii ni ..... Kutekeleza amri / maagizo unayopatiwa kwa unyenyekevu.

Ingawaje upendo pengine sio lazima, lakini utii wa kweli wa kutoa matunda yake ni lazima uwe ni utii kwa Ikhlas / upendo.

Maana ya Nidhamu ni ..... Utaratibu uliowekwa wa kufanyika kwa jambo fulani kwa mafanikio..

NIDHAMU YA UKHALIFA

Ukhalifa ni Muongozo wa Islam uliofundishwa katika Quran Tukufu ambapo waaminio kwa kujiweka chini ya mkono wa Khalifa (akiwa mwakilishi wa Allah duniani) wanatekeleza majukumu ya kutimiza lengo la Mwenyezi Mungu kuwaweka wanadamu hapa duniani.

Ukhalifa huu umeahidiwa katika Quran:

Allah Amewaahidi wale waliomaini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, bila shaka Atawafanya makhalifa katika ardhi kama Alivyowafanya makhalifa wale wa kabla yao (24:56)

Pia Mtukufu s.a.w amesema

Hadithi ya ukhalifa:

Kisha utakuwepo ukhalifa chini ya misingi ya unabii (Musnad Ahmad).

Akieleza umuhimu wa Ukhalifa, Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad, Khalifatul Masih II anasema:

Mungu Mwenyezi hufanya kila kitu kwa hekima na kuona mbali, na daima kuna sababu nzuri na mantiki nyuma yake. Kulingana na sheria za asili za asili, mwanadamu ana muda mdogo tu wa maisha, lakini kazi ya matengenezo na mafunzo ya jamii inahitaji mengi .Kwa hivyo, Mwenyezi Mungu ameweka mfumo wa Ukhalifa baada ya mfumo wa Utume, Khalifah anaendelea na kuendelea na kazi ya Mtume. Mbegu iliyopandwa na Mtume inalindwa na kukuzwa na Khalifah mpaka inakuwa mti imara.

Hii inaonyesha kwamba kwa hakika Ukhalifa ni chipukizi au tawi la mfumo wa Utume ndiyo maana Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) anasema kwamba baada ya kila Mtume mfumo wa Ukhalifa unawekwa.

Hakuna Mtume ambaye hajafuatwa na Ukhalifa.

Mafundisho ya Kiislamu kuhusu uteuzi na hadhi ya Khalifah ni kwamba ofisi ya Ukhalifa haiwezi kurithiwa kwa hali yoyote. Bali, Ukhilafat ni amana takatifu ambayo imekabidhiwa kwa mjumbe mchamungu wa Jumuiya kupitia uchaguzi. Uislamu zaidi - unafundisha kwamba ingawa Khalifah anateuliwa kwa njia ya uchaguzi, kwa hakika, Mwenyezi Mungu Mtukufu anawaongoza wanachama kuelekea kwenye uchaguzi wa mtu mwema na mwenye uwezo kama Khalifa.

Pindi mtu anapochaguliwa kuwa Khalifah, basi kwa mujibu wa mafundisho ya Kiislamu, wanajamii wote wanatakiwa kumtii kikamilifu. Wakati huo huo, inatakikana kwamba Khalifah atekeleze majukumu yake kama Khalifah kwa kushauriana na kutilia maanani maoni ya wanachama. Hata hivyo, si wajibu kwake kukubali daima maoni na mapendekezo ya wanachama.

Khalifatul Masihi (mrithi wa Masihi Aliyeahidiwa na Mahdi as) anachaguliwa kwenye ofisi hiyo kwa kupigiwa kura na wajumbe wa Chuo cha Uchaguzi, ambacho kilianzishwa kwa ajili hiyo na Hadhrat Musleh Mauud ra. Chuo cha Uchaguzi kinafanya kazi chini ya usimamizi wa Khalifa. Hata hivyo, baada ya kufariki kwa Khalifa, Chuo cha Uchaguzi kinakuwa huru kabisa na kumchagua Khalifa ajaye.

Khalifatul Masih ndiye Kongozi Mkuu wa Jumuiya katika maswala yote ya kimwili na kiroho.

Kama Kiongozi Mkuu wa Jumuiya, Khalifatul Masih anaongoza na kuongoza shughuli za Jumuiya, na taasisi na jumuiya zote ndani ya Jumuiya ziko chini yake.

Wanajumuiya wote wanawajibika kumtii baada ya kuwa wamefanya hadi ya Baiat kwa mkono wake.

Yeye ni Baraka kubwa kutoka kwa Allah na kupitia yeye kila mwanajamaat hujipatia muongozo na mwanga wa kiroho. Kwa hekima ya Allah yeye huyajali na kujitahidi kuyatatua matatizo yote yamuhusuyo mwanajmaat mmoja mmoja na wote kwa ujumla katika maisha yao ya kila siku.

Muundo wa Uongozi wa Jamaat Ahmadiyya uliopo kwa sasa ni kama ifuatavyo:

Khalifatul Masih

Majlis Mushwarat (Shura ya Kimataifa na Shura za Mataifa)

Sadr Anjumah Ahmadiyya (Makao Makuu Rabwah)–

Tahrik Jadid Anjuman Ahmadiyya (Mpango Mpya)

Waqfu Jadid

Local Ajumans

Sadr Anjumah Ahmadiyya (Makao Makuu Rabwah)–

Ilianzishwa na Masihi Aliyeahidiwa mwenywe

Endelea uk 4

Amri ya utii wa Nidhamu ya Jamaat

Chini yake kuna Nazarat (Idara mbalimbali)
Kiongozi wa Idara anaitwa Nazir
Kongozi wa Sadr Anjumah Ahmadiyya anaitwa Nazir Aaala ambaye anafanya kazi chini ya Miongozo na Maelekezo ya Hadhrat Khalifatul Masih atba
Nazarat Mbalimbali zipo mfano: (16)
Nazarat Ulya – Idara Kuu
Diwan – Watumishi taarifa zao, posho zao, upandaji vyeo na
Baitul Maal Amad (Iadara ya Fedha na Mapato)
Baitul Maal Kharch (Idara ya Fedha na Matumizi(
Umur Aaama (Mambo ya Ndani ya Jamaat)
Islahu Irshaad Markaziyya (za Ziada)
Taalim
Ziraat
Sanau Tijaarat
Khidmat Darweshaan (For Qadian Affairs)
Daaru Dhiafat
Ishaat wa Tasneef
Umur Khaarijah

Katika Baadhi ya Nazaarat zipo Nadhaamat (Vitengo) ambapo mkuu wa Kitengo huitwa Nazim. Eg Nazim Tashkhiis Jaidad
Nazim Daru Ifta nk

Tahrik Jadid Anjuman Ahmadiyya (Mpango Mpya)
Wakaalat (Mkuu Wakil Aala)
Wakaalat Taalimu Tanfidh (Utekelezaji wa Mipango yote)
Wakaalat Diwaan (Mapato)
Wakaalat Tabshir (Wakilul Tabshir - Foreign Missions(
Wakaalat Maal (Wakilul Maal) (Awwal na Thaani, Thalith)
Taalim
Tasnif
Waqfu Nau
Sanaut Tijarat
Ziraat

Waqf Jadid
Nizamat Maal
Nizamat Irshaad (Religious Training of Muallimiin)
Fadhl Umar Free Homoepathic Dispensary

Local Anjumans
National HQs – (National Majlis Amila
Amir
General Secretary
Secretary Tablīgh (Preaching)
Secretary Tarbiyat (Religious Training)
Secretary Talīm (Education)
Secretary Ishāat (Publications)
Secretary Ishāat Samī wa Basarī)Audio and Visual(
Secretary Umur Kharijiyya (External Affairs)
Secretary Umur Amma (General Affairs)
Secretary Diyāfat (Hospitality)
Secretary Māl (Finance)
Secretary Tahrīk Jadīd
Secretary Waqf Jadīd
Additional Secretary Tarbiyat and Waqf Jadīd Nau Mubaiīn (for New Ahmadīs(
Secretary Jāidād (Properties)
Secretary Waqf Nau
Secretary Zirāat (Agriculture)
Secretary Sanat-o-Tijārat (Industry and Trade)
Secretary Tajneed

Aidha katika kusaidia majukumu ya Jamaat, kuna pia utaratibu wa Tanzeem ambapo Uongozi kutoka Makao makuu hadi matawini pia unakuwepo.

Hivyo ni muhimu bali ni lazima kujiunganisha na mlolongo huu wote ili kutimiza falsafa nzima ya utii.
Hii ni sawa na hadithi ya Mtume s.a.w.
Wa man atwaa Amiirii faqad atwaanii, waman aswaa amiirii faqad aswaani) Masnad Abii Daud.(
Yaani yule aliyemtii Amiri niliyemteua basi huyo amenitii mimi na yule aliyemuasi Amiri niliyemteua basi huyo ameniasi mimi.

Huu ni mnyororo, ni kama mti, ni kama mwili, ni kama akili, bila ya kushikamana na kuunganika wote unapoteza maana yake yote.

KUJITOLEA MALI...
Ni Agizo la Mwenyezi Mungu katika aya Mbalimbali

Aya chache

Hadithi chache

Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema:
Yeyote anayenisaidia katika maisha yangu katika mahitaji yangu ya kidini kwa mujibu wa maelekezo yangu, InshaAllah atakuwa nami huko Akhera. Siamini kwamba yeyote anayetumia mahitaji haya muhimu ya kidini atapata kupunguzwa kwa mali yake, bali itapungua. ubarikiwe kwa wingi. Ukiwa na imani kamili kwa-Mwenyezi Mungu, unapaswa kutenda kwa ujasiri na ujasiri.Huu ni wakati wa kutumikia imani. Wakati utakuja ambapo hata mlima wa dhahabu hautalingana na senti moja inayotumika sasa.
Huu ni wakati wa baraka kama nini! Yule aliyewekwa rasmi na Mungu, ambaye mamilioni walikuwa wamemngoja kwa karne nyingi, yuko miongoni mwenu. ... Aya kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu zimebainisha wazi kuwa ni wao tu watakaohesabiwa kuwa ni watu wa umma wanaotumia pesa zao.
Usifikiri kwamba unapata mali yako kwa uwezo wako mwenyewe; ni baraka za Mungu. Usifikiri kwamba kwa kutumia sehemu yake unafanya upendeleo kwa Mungu; bali ni kibali cha Mungu juu yako kwamba amekuita uitumikie imani yake.
…
Ni dhahiri kwamba huwezi kupenda vitu viwili; haiwezekani ukapenda mali yako na kumpenda Mungu. Unaweza kumpenda moja tu. Kwa hiyo, mwenye bahati ni mtu anayempenda Mungu. Ikiwa yeyote kati yenu atampenda Mungu halafu anatumia mali katika kazi yake, naamini kabisa kuwa mali yake pia itabarikiwa kuliko wengine kwa sababu mali haiji yenyewe, huja kwa mapenzi ya Mungu.
Kwa hivyo, yeyote anayetoa sehemu ya mali yake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu - bila shaka atarudishiwa. Lakini yeyote ambaye hatumikii njia ya Mwenyezi Mungu kwa sababu ya kupenda mali yake, basi atapoteza mali hiyo.

Kwa kifupi zipo faida 2 kubwa za Kujitolea Mali...
1. Kuzalisha utakaso wa kutokuiangukia Dunia na starehe zake kwa anayejitolea mali yake (Zakat)
2. Kusaidia mipango Kadhaa ya Jamaat iende mbele (itekelezeke(

Utaratibu tulionao leo wa kujitolea Mali (Chanda)...
Chanda ni michango ambayo kila Ahmadiyya analazimika kulipa, kwa mujibu wa kanuni zilizowekwa na Masihi Aliyeahidiwa na Mahdi as na Makhalifa wake.
Baadhi ya Chanda ni wajibu, na nyingine ni za hiari. Chanda za lazima zina kiwango maalum na lazima zilipwe kwa kiwango kilichowekwa. Hata hivyo, wale wanachama ambao wanakabiliwa na matatizo ya kifedha wanaweza kutoa Chandas za lazima kwa kiwango kilichopunguzwa, lakini tu baada ya kupata ruhusa ya Khalifa tul Masih.

Aina za Michango
Zakat – Quran tukufu – Sawa na Viwango vyake
Fitrana – Mtukufu Mtume s.a.w. (Sa'a (pishi) Moja) (fedha– (Chakula cha kumtosha mtu mmoja wakati wa Eidul Fitri
Chanda Aam (1/6), Chanda Wasiyyat (1/3 (1/10 – na Chanda Jalsa Salana – Masihi Aliyehaidiwa a.s.
Tahrik Jadid (1934) (Nov. 1 – Oct. 31) sawa na ahadi
Waqfu Jadid (1957), (1 Jan31 – . Dec – (ahadi
Eid Fund
Sadaqa
Buyuutul Hamd – Mosque Fund
MTA Fund – Satelite Fund
Darul Yataam Fund
Mariyam Fund n.k

Hoja ya kuumba kwa Nabii Issa[as]

Mwandishi akiendelea ana sema Isa ndani ya Qurani Kaumbwa kama alivyo umbwa Adam 3:60 Bila shaka hali ya Issa kwa Mwenyezi Mungu ni kama hali ya Adam aliumbwa kwa udongo kisha akamwambia kuwa basi akawa .Akifafa nua alivyo elewa muandishi wa Bibli ni jibu anasema Hivyo kwa mujibu wa ayah ii Issa aliumbwa kama alivyo umbwa Adam yani kwa udongo na kama Adam alivyo tenda dhambi ndivyo na Issa alivyo mwisho wa kunukuu.
Kwa hali hiyo inaonesha jinsi gani mwandishi alivyo kua haelewi Qurani na hilo sio ajabu . kwani Mwenyezi Mungu Anasema katika sura 47-17:46;Na unapo soma Qurani tunatia baina yako na baina ya wale wasio aminin Akhers pazia iliyo sitiria . Natumetia vifuniko Mioyoni mwa asiye wafahamu. Na katika masikio yao kuna uzito na unapo mtaja mola wako wa pekee katik Quranibasiwaohugeuzamigongo yao kwa chuki huo ndio uhalisi . Kwani aya imeonyesa ni jinsi Issa alivyo patikana kwa kutumia neno la qun faya quni kama vile Adam alivyo kuwa kwa Mwenyezi Mungu alivyo sema kuwa akawa nafsi hai ndivyo na yesu alivyo patikana kisani nay eye aliambiwa kuwa tumboni akawa tumboni mwa mama yake Mariyam Ajabu eti mwandishi haelewi Mariyam . Ajabu eti mwandishi haelewi Nikwamba Mwenyezi Mungu alichokusudia hapo ni kuwepo kwao yani wote wawili kauli moja tu iliyo tumika ya kuwa kisha wakawa Yaani Adam hakuwa na wazazi yani hakuwa na baba wala mama hivyo uwepo wake ulitokana na neno la kuwa akawa katika mavumbi pia Issa hakuwa na baba na baba ndio huweka Mimba kwa mwanamke . Hivyo kwakuwa Mariam huku mjue mtu kwa mwanamkwe . Hivyo kwakuwa Mariam haku mjua mtu Mume Na yeye Mimba ilipatikana kwa neno la kuwa ikawa mimba huo ndio mfanano wa Issa na Adam na si vinginevyo

Ahmadiyya yakutana na viongozi wakuu wa Nchi

Hivi karibuni njia hiyo hiyo amekanyaga Khalifatul Masih wa (v) Hadhrat Masroor Ahmad[atba] ambaye amewaandikia viongozi wa Mataifa makubwa Duniani na viongozi wa Dini akiwafikishia ujumbe wa Islamu na namna Islam inavyoweza kusimamisha amani Duniani. Viongozi aliowaandikia ni pamoja na:- Waziri Mkuu wa Israel- Benjamin Netanyahu, Raisi wa Ufaransa- Emmanuel Macron, Raisi wa China- Xi Jinping, Chansela wa Ujerumani, Angella Merkel- Waziri Mkuu wa India Narendra Modi, Waziri Mkuu wa Japan- Shinzo Abe, Waziri Mkuu wa Urusi- Vladmir Putin, Waziri Mkuu wa Uingereza- Boris Johnson, Raisi wa Marekani- Donald Trump, Waziri Mkuu wa Canada- Justin Trudeau.

Kwakufuatanyayonamifanoyotehiyoiliyotukuka Amir na Mbashiri Mkuu wa Tanzania Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry akiongozana na ujumbe wa Naibu Amir, Sheikh Abdul-Rahman Muhammad Ame, Sheikh Khawaja Muzaffar Sahib pamoja na Yahya Y. Kambaulaya Sahib-Katibu wa Umur Amma Taifa. Walimtembelea Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Mjini Dodoma na kuwa na mazungumzo naye Makao Makuu ya Nchi Dodoma. Waziri Mkuu alishukuru zawadi aliyopewa ya Kuruani Tukufu na alisifu juhudi za Jumuiya ya Ahmadiyya katika kutoa huduma kwa







Jamii hususani katika nyanja za Elimu, Matibabu, usambazaji wa umeme wa Jua na ujenzi wa visima ili kuwapatia Wananchi Maji safi na Salama. Waziri Mkuu Alipewa mwaliko wa kuhudhuria Jalsa Salana, lakini kutokana na sababu za nje ya uwezo wake, aliahidi kumtuma mwakilishi Waziri Sera, Bunge na Uratibu-Mh. George B. Simbachawene.

Ujumbe wa pili ulionana na Makamu wa Raisi Dr. Isidore Mpango Mjini Dar es Salaam, ulioongozwa na Naib Amir Sheikh Abid Bhatti na Naib



Amir Sheikh Abdul-Rahman M. Ame. Wengine katika ujumbe Alikuwa ni Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Ahmadiyya Tanzania, Seif H. Nakuchima Sahib na Sheikh wa Mkoa wa Dodoma Muzaffar Khawaja Sahib.

Makamu wa Raisi alifurahi kupokea ujumbe huo na ujumbe wa Jamati uliomueleza Hisitoria fupi ya Ahmadiyya Nchini na Kumkabidhi Kuruani Tukufu na Gazeti la Mapenzi ya Mungu, Makamu wa Raisi alipokea zawadi hizo kwa furaha na heshima kubwa. Aliomba pia nakala za nyuma za gazeti la Mapenzi ya Mungu, Makamu wa Raisi alisifu juhudi za Jumuiya kuendeleza Kiswahili, hususani Tafsiri ya Kurani Tukufu kwa Kiswahili. Alipokea kitabu cha Yesu katika India. Alitabasamu na kusema ama kweli elimu ni bahari pana.





Ujumbe wa tatu, ukiongozwa na Amir na Mbashiri Mkuu wa Maulana sheikh Tahir Mahmood Chaudhry. Ulitembelea Bunge la Tanzania mjini Dodoma na kukutana na Spika wa Bunge hilo Dr. tulia Ackson. Spika Tulia aliwapokea vizuri kwa kulieleza Bunge juu ya ugeni huo wa Jumuiya ya Ahmadiyya Tanzania, ambayo ilisajiliwa Mwaka 1936. Baada ya maelezo hayo alimkabidhi Kuruani Tukufu na baadhi ya vitabu vya Jamati vikiwemo vya Karafuu Zanziba.



Jamati ilimaliza vizuri Mwaka kwa kutua kwenye visiwa na kukutana na Raisi wa Tanzania Dr. Samia Suluhu Hassan. Ujumbe mzito wa kukutana na Raisi, uliongozwa na Amir na Mbashiri Mkuu Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry, Naib Amir Abid Bhatti na Naib Amir Sheikh Abdul-Rahman Muhammad Ame, Katibu Mkuu wa Jamati Tanzania Seif Nakuchima Sahib, Sadr Majlis Lajna Bi. Zena Nyange. Jambo lililowapa faraja wawakilishi wa Jamati ni kauli ya Raisi, kuwa amewahi kusoma baadhi ya vitabu vilivyotolewa na Jamati Ahmadiyya.



Bustani ya Washairi

Kasida ya kumsifu Mtume Mohamed (saw)

16

فتهللوا بجواهر الفرقان نهب اللئام نشوبهم وعقارهم

Tafsiri: Watu waovu walipora mali zao na milki zao lakini wakang'arika kutokana na johari za Kurani Tukufu.

Maelezo: Makafiri waliendelea na maonevu yao ya aina mbalimbali dhidi ya Waislamu. Walinyang'anywa mali zao na walipata mateso ya aina aina. Hata hivyo, waliendelea kuvumilia shida zote kwa kumtegemea Allah subhanahu wataala. Jambo hili likawasababisha wafikie kiwango cha juu cha Taqwa na UchaMungu. Waliamua kuifuata Kurani Tukufu na kwa sababu ya nuru yake nao waling'aa kama nyota za ardhini.

17

لتمتع الإيقان والإيمان كسحوا بيوت نفوسهم وتبادروا

Tafsiri: Walitakasa makao ya roho zao na wakatoka ili kufaidika na yakini na Imani

Maelezo: Mateso na shida zikaongezeka kwa ajili ya masahaba lakini walionesha mfano wa kuiga kwa watu wote. Masahaba waliamua kuuondoa uchafu wote kwa kusafisha undani wa mioyo yao. Jambo hili liliwanufaisha kiasi kwamba walipata nuru ya Imani ing'arishe roho zao.

18

كالعاشق المشغوف في الميدان قاموا بإقدام الرسول بغزوهم

Tafsiri: Kwa sababu ya kutoka kwa Mtume, walisimama imara katika medani kwa ajili ya vita vyao kama mshabiki aliye na huba nyingi

Maelezo: Masahaba walipata bahati kubwa ya kuwa mstari wa mbele katika kumsaidia Mtume Mtukufu (saw) ndani ya Maisha yake. Kila alipotoka Mtume (saw) katika njia ya Allah subhanahu wataala ili kuihami dini yake basi hali ya masahaba ilikuwa pia ya mfano. Si tu walimwitikia vizuri Mtume Mtukufu (saw) bali walisimama kidete kwa sababu walimpenda sana Mtume Mtukufu (saw) na hakuna aliyeweza kuutoa upendo huu nje ya nyoyo zao.

19

تحت السيوف أُريق كالقربان فدم الرجال لصدقهم في حبهم

Tafsiri: Hivyo damu ya watu ikamwagiwa chini ya panga kama dhabihu kwa sababu ya uhalisi wa upendo wao

Maelezo: Masahaba wa Mtume Mtukufu (saw) walionesha ikhlasi na moyo wa upendo kiasi kwamba hawakusita kujitolea mhanga njiani kwa Allah. Sababu pekee iliyowapelekea kufanya hivi ni mahaba na upendo kwa Mola wao na Mtume wake (saw). Kutokana na upendo huo hawakujali hata maisha yao bali walitoka kifuambele ili kuitetea dini tukufu ya Uislamu.

20

فسترتهم بملاحف الإيمان جاؤوك منهوبين كالعريان

Tafsiri: Walikujia wakiwa wamenyang'anywa (mali yote) kana kwamba walikuwa rabana nawe ukawafunika kwa mashuka ya imani

Maelezo: Masahab a walipojiunga na dini tukufu ya Uislamu waliachwa peke yao na ndugu na jamaa zao. Kwa kweli hali hii ilikuwa ngumu kwao kana kwamba walinyang'anywa mali yao yote. Lakini waliendelea kupata maarifa ya kidini kwa Mtume Mtukufu (saw) walipata nuru ya imani iliyowafunika na kuwatunza. Nuru hii ilisababisha wamkurubie Allah subhanahu wataalaa na wakapewa jina la *Ashabii kan-nujuum*.

Na.
Shahab Ahmad
Morogoro, Tanzania

KIBURI SI MAUNGWANA

Ili ujifunze mengi, Ishi na watu vizuri,
Utaikosa misingi Ukijifanya kiburi,
Acha sifa ya kigingi,Mola hapendi kiburi,
Kiburi si maungwana, Chondechonde chunga mwana.

Kiburi si maungwana,Wahenga walishasema,
Chondechonde chunga mwana,Usije pata kilema,
Kuwa na sifa mwanana,Yenye kusifika vema
Kiburi si maungwana, Chondechonde chunga mwana.

Sifa njema ni silaha, ya upendo maishani,
Ifanye kuwa jeraha,Lisilopona mwilini,
Utaipata furaha,Popote pale nchini,
Kiburi si maungwana Chondechonde chunga mwana.

Nne ni yaukingoni,Namshukuru karima
Sina mengi ya mizani,Hapo ndipo nimekoma
Nisemayo si utani,wala usirudi nyuma
Kiburi si maungwana Chondechonde chunga mwana

Saliana Higiro

DHAHABU YA KUSINI:

1. Nakuomba Maulana, uniongoze
   Nikiwa bado kijana, nijitulize
   Nifanye vyenye maana, nisizogoze
   Rabbi taqabbal Du'a, nihifadhie

2. Sina uwezo wowote, wa kuilinda
   Itanibidi nijute, ikinishinda
   Sijivunii chochote, nisijekonda
   Rabbi taqabbal Du'a, nihifadhie

3. Ikitokeza juani, yameremeta
   Inawindwa na wahuni, wapiga ngeta
   Nikisema kulikoni, wananipeta
   Rabbi taqabbal Du'a, nihifadhie

4. Nikihifadhi kizani, yametameta
   Wanasema hiko nini, yamenikuta
   Ninajishika kichwani, nasikitika
   Rabbi taqabbal Du'a, nihifadhie

5. Ninakuomba Rabana, unilindie
   Si usiku si mchana, iangalie
   Mana inang'ara sana, isipotee
   Rabbi taqabbal Du'a, nihifadhie

6. Kuomba siwezi acha, maisha yangu
   Hata kama kumekucha, kanuni yangu
   Na mimi sio ndondocha, imani yangu
   Rabbi taqabbal Du'a, nihifadhie

7. Mungu wangu Mungu wangu, unibariki
   Bado naona uchungu, wa wazandiki
   Bado Dhahabu ni yangu, wanahamaki
   Rabbi taqabbal Du'a, nihifadhie

8. Bado ninaifunika, isiponyoke
   Watu wataka ipoka, waburudike
   Kukuomba sijachoka, unikumbuke
   Rabbi taqabbal Du'a, nihifadhie

9. Sina ujanja wowote, wa kuitunza
   Na wahuni kama wote, wataniponza
   Ninafata njia zote, za kuitunza
   Rabbi taqabbal Du'a, nihifadhie

10. Dhahabu ninayo ndogo, siipotezi
    Vijana hawana dogo, wana uchizi
    Wasije nipa kisago, cha upekuzi
    Rabbi taqabbal Du'a, nihifadhie

11. Ngoja wapate za kwao, washuhudie
    Leo kwangu kesho kwao, wasijutie
    Hii yangu sio yao, wasiumie
    Rabbi taqabbal Du'a, nihifadhie

12. Shida yenu ipo wapi, inashangaza
    Ni Dhahabu sio pipi, ninawajuza
    Vya watu hamuogopi, mnajiliza
    Rabbi taqabbal Du'a, nihifadhie.

13. Sina ujanja wowote, wenye kiburi
    Kukuomba kama kote, ndio Kahari
    Nangu mipa si chochote, si mtabiri
    Rabbi taqabbal Du'a, nihifadhie

14. Nitunzie hii kitu, nijivunie
    Mimi hapa kama mtu, nikumbatie
    Na roho zao za kutu, wahurumie
    Rabbi taqabbal Du'a, nihifadhie

15. Kwa leo ninasitisha, nimekomea
    Misuli nimetunisha, najihemea
    Sio kama nawatisha, mtapotea
    Rabbi taqabbal Du'a, nihurumie.

Abdallah S. Kalindima(CHUMACHAKAVU)
Dar es Salaam

Acha dharau

Mwenzangu dharau acha, kesho yako hujajua
Wamwona kama kikucha, kesho utamlilia
Wengine wameuficha, ubora usotambua
Wakati takapo kucha, usije ukajutia
Mwenzio sijayaficha, tayari menikutia
Na hapa mefika ncha, nakuhasa yashikia.

Masihi Omary Stambuli kisagwa

HABA JANA_

1. Rabu nashika Kalamu, Kichwani tenzi sina
   Kuidondosha haramu, Vidole vinakwazana
   Hi safari sina hamu, Rabu tupe suluhisho

2. Safari nimeianza, Navuta pumzi joto
   Kauli zinanipinza, Pekua njia kokota
   Hi safari sina hamu, Rabu tupe suluhisho

3. Weka hatua Jasiri, Sauti mwangwi yanadi
   Shari siriye safari, fumbo ongeza juhudi
   Hi safari sina hamu, Rabu tupe suluhisho

4. Kusafiri sina budi, umuhimuwe najua
   Wengi waacha kusudi, ili tushindwe ng'amua
   Hino safari Waqfu, Ni ngumu tundale tamu

Shunda Mshundia Wana
Daluni, Tanga
+255656557721

NAOMBA

Naomba yako huruma, Rabi uliyeniumba
Uniepushe Zahama, Imara nisije yumba
Chini ya yako Rehema, univunike Wa Mamba
Huo ndio ufaulu, katika haya maisha.

Mahmood Hamsin Mubiru(Wa Mamba)
Migombani, Kiwalani

Kutoka Uk. 01

Ahmadiyya alitembelea jengo la ofisi za Ansarullah. Mradi huu wa jengo ambao umeanza kujengwa mwaka 2018 huu ni mwaka wa tano wa ujenzi huo. Amir sahib alijionea jengo kubwa na zuri japo halijakamilika lakini aliridhishwa na harakati zote za ujenzi huo hadi pale tulipofika katika hatua



za kupaua bati. Jengo lina vyumba 7, vyoo, ofisi, ikiwemo ofisi kubwa ya sadr majlis. Kuna store, jiko, vyoo vya ndani, chumba cha kupumzika na ukumbi mkubwa wa kuweza kuchukua watu 200. Hakika ni jengo hasa lenye kuonesha hadhi na heshima ya Tanzim ya Majlis Ansarullah. Amir sahib aliongoza maombi ya kimya kimya katika jengo hilo.



Katika hotuba yake ya kufunga Ijtimaa, Amir sahib aliwakumbusha Ansarullah juu ya malezi hasa kwa vijana kwa Ansarullah kuwa mfano kwao wa kuigwa. Kama Ansarullah hatutokuwa na tabia njema, tutambue hata Watoto hawatokuwa na sehemu ya kujifundisha tabia njema. Akakumbusha juu ya kiapo cha Tanzim kuwa tukisome kwa kumaanisha. Kupitia maneno na matendo yetu, tuweze kuwaita wengine kwetu. Pia Amir aliwakumbusha Ansarullah juu yas kukamilisha mchango wa wakf Jadid ikizingatiwa kuwa huu ndio mwezi wa mwisho.

Katika ijtimaa ya mwaka huu, idara ya maonesho iliandaa maonesho mazuri kabisa na ya kuvutia. Mabango ya picha za matukio yaliyofanyika kwa mwaa mzima yalioneshwa. Kulikuwa na mauzo ya vitabu vya jamaat, saa nzuri zenye picha za Masih na makahalifa wake, kalamu zenye nembo ya Majlis Ansarullah na Tshirt nzuri za Majlis Ansarullah zilipendezesha maonesho hayo.

Hakika ijtimaa ilikuwa nzuri na iliyopangiliwa vizuri sana. Mwisho wa Ijtimaa ilipigwa picha ya pamoja kwa wahudhuriaji wote.

MajlisAnsarullahnitandhimyawanaume wenyeumriwamiaka40nakuendelea. Katika Ijtimaa ya mwaka huu, takriban watu 209 wakiwemo ansarullah 188 kutoka mikoa 15 ya Tanzania walihudhria na khuddam 21 waliokuja kutoa baadhi ya huduma katika Ijtimaa hiyo.

Mwenyezi Mungu Atubariki na atujaalie uwezo wa kufuata mafundisho sahihi ya Islam chini ya kivuli cha Khilafat Ahmadiyya. Amin



TAFUTA MANENO

Tafuta maneno 24 hapo chini kwa kuyazungushia na Penseli

N	C	G	M	A	P	I	N	D	U	Z	I	M	K	L	M
T	L	N	L	B	G	L	B	W	S	G	L	R	J	N	A
S	P	M	I	B	U	G	H	U	D	H	A	L	D	L	H
H	Y	L	M	S	S	M	K	N	B	L	A	K	M	U	A
U	W	J	L	E	A	A	D	I	P	I	I	I	R	H	R
R	Z	L	P	N	J	B	L	G	S	H	L	A	R	K	I
A	Y	K	R	S	H	V	X	A	S	U	B	E	M	I	M
M	V	J	D	A	M	J	V	I	N	U	D	U	S	G	U
B	W	E	R	E	R	E	L	L	R	A	B	A	M	H	M
A	N	D	G	R	T	I	A	A	U	A	L	J	A	D	I
F	W	I	Y	R	K	O	B	K	L	A	M	A	U	K	G
R	F	F	D	A	K	R	U	A	G	D	L	N	D	K	N
I	L	F	R	A	M	B	H	N	G	F	B	N	H	F	D
T	J	A	R	F	H	G	U	K	R	L	D	A	M	N	T
I	T	A	Z	T	A	B	L	B	Z	B	U	R	A	H	I
Q	B	R	I	S	I	T	I	M	A	J	I	L	I	S	I

Tarakilishi	Shairi	Barubaru	Afriti
Bughudha	Maud	Bwerere	NIDA
Bileshi	Barakoa	Kisu	Buku
Sensa	Risiti	Janna	Majilisi
Aghalabu	Salana	Mapinduzi	Nisab
Burahi	Maharimu	Bungala	Shura

UNGANISHA NUKTA

Unganisha nukta ili upate picha moja iliyokamilika.





Jinsi ya Kupika Pilau la Nyama

Orodha ya Viungo

Mchele kilo1 ¼
Nyama kilo ½
Mafuta yakupikia lita ¼
Njegere kilo ½
Giligilani pakti ndogo 1
Mdalasini ya unga packti ndogo 2
Jira packti ndogo 2
Chumvi packti ndogo 1
Vitunguu-maji kubwa 3
Vitunguu-saumu kubwa 1
Hatua ya kutayarisha viungo
Ukisha andaa vitu vyote hivi tunaanza kuandaa chakula chetu cha Leo
Anza kumenya vitunguu saumu
Katakata vitunguu maji
Chambua girigilan
Kata kata nyama
Chukua vitunguu swaumu, girigilan, jira viweke kwenye kiuri na utwange vizuri hadi vilainike
Hatua na maelekezo ya kupika
Chukua sufuria yako bandika jikoni weka mafuta
Weka vitunguu maji jikoni
Kaanga hadi viwe na ranging ya kahawia
Weka nyama anza kuikaanga
Endelea kugeuza nyama yako ikaange vizuri hadi iive
Chukua mchanganyiko wa vitunguu swaumu, girigilan, jira ulio twanga viweke na endelea kukaanga
Chukua mdalasin weka koroga vizuri
Weka chumvi geuza
Weka njegere zako geuza vizuri ichanganyike
Weka maji acha ichemke kwa dakika tano
Weka mchele geuza vizuri tara-araatibu
Funika na uweka moto mdogo wakuivisha chakula taratibu kwa dakika kumi
Funua chakula chako geuza hapo kitakua pilau iliyo tayari kwa kula
Hitimisho na Mawasiliano ya Mwandishi
Kwa kuhitimisha napenda kusema tu kwamba upishi wa pilau uko wa aina nyingi na hata ndani ya aina moja bado mapishi yanaweza kutofautiana sana na inategemea Zaidi ubunifu wa mpisha kuweza kupindisha pindisha baadhi ya taratibu ili kuweza kupata chakula kizuri, kitamu na kinachowavutia walaji.
Mfano tu kwenye pilau ya nyama unaweza weka nyama nyingi, kawaida au chache, unaweza kubadilisha rangi ikawa kahawia au njano nk



Hakuna Atayewashinda

Na. Mwandishi wetu

Allah alimuahidi mtumishi wake Hazrat Mirza Ghulam Ahmad[as] kuwa, wafuasi wake watapewa ujuzi wa mambo na maarifa kiasi ya kwamba, watawanyamazisha wapinzani na maadui wao.

Kila hoja wataivunja kwa hoja iliyokuwa bora Zaidi, na kila uzushi utapotea kama vile Moshi unavyopotelea angani Ismail Ahmad Mpukutile alikuwa Mwenyekiti wa chama cha Ushirika mkoani Lindi. ushirika huo kwa jina la kigeni ulijulikana kama Lindi Regional Co-operative Union. Wasomi na wabahaisha wote nchini walivamia vyama hivi na kwa kutumia ujanja wao wa mahesabu wakaviacha hoi vyama hivyo. Mkoa wa Lindi haukupona katika mashambulio hayo. Pesa zililiwa tena zililiwa kweli kweli. Meneja wa ushirika akawa na kesi ya kujibu na Mwenyekiti akatakiwa atoe utetezi wake. Meneja wa ushirika aliposimama mbele ya hakimu akaanza kumimina ung'eng'e. Hakimu alikaa kimya na alipomaliza, ikawa zamu ya Ismail Ahmad Mpukutile. Naye hakuwa nyuma kiarabu alichokuwa anakijua naye akamwaga huku moyoni akisema kuwa *kama mbwayi mbwayi*. Hakimu alisikiliza, kilikuwa ni kigiriki kitupu kwake baada ya kutafakari kidogo akatoa uamuzi kwamba maelezo toka pande zote mbili yatolewe katika Kiswahili. Hili lilitekelezwa na kesi ilimuendea vibaya Meneja na akafungwa kwa kufuja pesa za wanaushirika. Tizama hekima aliyotumia Mzee Ismail Ahmad Mpukutile ni baraka za kumpokea Masihi aliyeahidiwa[as].

Silaha ambayo Meneja ushirikia, iliyotaka kutuma kuangamiza, alipoitumia Mzee Mpukutile ilileta. Mahakamani kuthibisha usemi wa Kurani Tukufu walifanya hila na Mwenyezi Mungu ni Mbora wa wafanyao **HILA.**

NUKUU YA LEO

وعن أبي سَعيد سعدِ بن مالكِ بن سنانٍ الخدري رضي الله عنهما: أَنَّ نَاسًا مِنَ الأَنْصَارِ سَأَلوا رسولَ الله صلى الله عليه وسلم فَأَعْطَاهُمْ، ثُمَّ سَأَلوهُ فَأَعْطَاهُمْ، حَتَّى نَفِدَ مَا عِندَهُ، فَقَالَ لَهُمْ حِينَ أَنْفَقَ كُلَّ شَيءٍ بِيَدِهِ: ((مَا يَكُنْ عِنْدِي مِنْ خَيْرٍ فَلَنْ أَدَّخِرَهُ عَنْكُمْ، وَمَنْ يَسْتَعْفِفْ يُعِفهُ اللهُ، وَمَنْ يَسْتَغْنِ يُغْنِهِ اللهُ، وَمَنْ يَتَصَبَّرْ يُصَبِّرْهُ اللهُ. وَمَا أُعْطِيَ أَحَدٌ عَطَاءً خَيْرًا وَأَوْسَعَ مِنَ الصَّبْرِ)). مُتَّفَقٌ عليه.

Abu Said Khudri r.a. anasimulia kwamba Mtume s.a.w. alisema:
Watu fulani miongoni mwa Ansar walimuomba Mtume s.a.w. awape chochote naye akawapa;
Wao wakamuomba tena naye akawapa hata akamaliza vyote alivyokuwa navyo mkononi.
Hapo akawaambia mali yoyote iliyonifikia sijawanyima.
LAKINI ANAYEJIEPUSHA KUOMBA OMBA MWENYEZI MUNGU HUMUHIFADHI.
Na anayefanya subira Mwenyezi Mungu Humpa subira (na kumtajirisha kwa subira) .
Na hakupewa mtu kitu bora zaidi kuliko SUBIRA.
(Bukhar na Muslim).

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA[as]

MWELEKEO WA MTU ALIYEKAMILIKA NA ATHARI YA MAOMBI YAKE

Ikiwa unataka kukubalika kwa Mwenyezi Mungu basi uwe na yakini na jambo hili na ufahamu hivi kwamba mikono yako, miguu yako, ulimi wako, macho yako, mwili wako wote na viungo vyako vyote kuwa ni masanamu tu yaliyoko njiani mwako; na miongoni mwa viumbe, vitu vingine vyote pia ni masanamu yaliyoko njiani mwako; watoto wako, mke wako na kila kusudio la kidunia ulitakalo na mali ya kidunia na heshima ya kidunia na staha za kidunia na kuitarajia na kuihofia dunia na kuwategemea Zaid na Bakari au kuhofia kuudhiwa na Khalidi na Walidi, haya yote ni masanamu yaliyoko njiani mwako.

Hivyo usiwe mtii wa sanamu lolote kati ya masanamu hayo, na usishughulikie kulifuata sana hata ukasahau vingine. Yaani, ulitunze sawa na haki za kisheria na suna za watu wema. Basi kama ukiisha fanya hivyo, wewe utakuwa kama kitu kipatikanacho kwa nadra, daraja lako litanyanyuka mno hata kwamba wewe hutaonekana, na Mwenyezi Mungu Atakufanya uwe mrithi wa Manabii na Mitume Wake; yaani elimu zao, maarifa yao na baraka zao ambazo zilikuwa zimefichikana na kutoweka utajaliwa upya na Uwalii utaishia kwako; yaani hatainuka yeyote baada yako atakayekuwa mkubwa kuliko wewe, na kwa dua zako, bidii zako na baraka zako, huzuni kubwa za watu zitaondolewa na mvua zitanyesha kwa waliokumbwa na njaa na mashamba yatastawi, na mabalaa na shida za kila mtu makhsus na wa kawaida hata masaibu ya wafalme yataondolewa kutokana na mwelekeo wako na dua zako. Na mkono wa kudra utakuwa pamoja nawe; popote utakapoelekea huo, nawe utaelekea huko. Na ulimi wa azali utakuita upande wake, yaani lolote litakalotamkwa na ulimi wako litakuwa limetoka kwa Mwenyezi Mungu na litawekewa baraka. Nawe utapewa daraja la wakweli wote waliopewa elimu kabla yako; na nguvu ya kuumba utajaliwa, yaani dua yako na mwelekeo wako utaleta mabadiliko ulimwenguni; hapo utakapotaka kukiletesha kisichokuwepo au kukitowesha kilichopo basi itakuwa hivyo hivyo, na mambo ya kimiujiza yatadhihirika kwako nawe utajaliwa kujua siri zilizofichika na elimu zitokazo Kwake na maarifa yasiyojulikana kwa wengine ambayo utafahamika kuwekewa amana na kuwa mstahiki. (Baraka za Dua, Footnote uk 31-30)

MATUKIO KATIKA PICHA



Picha ya pamoja ya Raisi wa Tanzania na wawakilishi wa Jumuiya ya Ahmadiyya -Ikulu Ndogo Zanzibar. Wa kwanza kulia akiwa ni Sadr Lajna Bi. Zena Nyange, wa pili Katibu wa Ummur Amma Taifa-Yahaya Y. Kambaulaya, wa tatu Naibu Amir Abid M. Bhatti, wa nne Raisi wa Tanzania Dr. Samia S. Hassan, wa tano Amir Sahib Sh. Tahir M. Chaudhry, wa sita Naibu Amir Sh. Abdul-Rahman M. Ame na wa saba Katibu Mkuu Seif H. Nakuchima.



Picha ya pamoja ya Spika wa Bunge la Tanzania na wawakilishi wa Jumuiya ya Ahmadiyya-Dodoma. Wa kwanza kulia akiwa ni Katibu wa Umur kharijiyya(Mambo ya nje)-Abillahi Kombo Sahib, wa pili Katibu Yahaya Y. Kambaulaya Sahib, wa tatu Naibu Amir Abid M. Bhatti Sahib, wa nne Spika wa Tanzania Dr. Tulia Ackson, wa tano Amir Sahib Sh. Tahir M. Chaudhry Sahib, wa sita Naibu Amir Sh. Abdul-Rahman M. Ame



Picha ya pamoja ya Makamu wa Raisi wa Tanzania na wawakilishi wa Jumuiya ya Ahmadiyya-Ikulu Ndogo Dar es Salaam. Wa kwanza kulia akiwa ni Sh. wa Mkoa wa Dodoma Khawaja Muzaffar Sahib, wa pili Naibu Amir Abid M. Bhatti, wa tatu Makamu wa Rais Dr. Philip Mpango, wa nne Naibu Amir Sh. Abdul-Rahman M. Ame na wa tano Katibu Mkuu Seif H. Nakuchima.



Picha ya pamoja ya Waziri Mkuu wa Tanzania na wawakilishi wa Jumuiya ya Ahmadiyya siku ya matembezi (Chamwino Dodoma). Wa kwanza kulia akiwa ni Katibu (Umur Ama) Yahaya Y. Kambaulaya, wa pili ni Sh. wa Dodoma Khawaja Muzaffar Sahi, wa tatu Amir Sahib Sh. Tahir M. Chaudhry, wa nne ni Waziri Mkuu wa Tanzania Mh. Kassim Majaliwa, wa tano Naibu Amir Abid M. Bhatti, wa sita Naibu Amir Sh. Abdul-Rahman M. Ame.



Kombe la Kabumbu Qatar 2022

Na. Mwandishi wetu

Mashindano ya kuwania Kombe la Dunia katika mchezo unaopendwa sana Duniani Kabumbu, yamemalizika nchi. Qatar tarehe 18/12/2022. Mambo mengi yalisimama. Mazungumzo. Mabishano. Kutambiana. Vyote hivyo vilikuwa hewani na kwa kufanya hivyo kuyaweka pembeni baadhi ya mambo muhimu katika Jamii. Ndio Ubinadamu wetu. Wepesi wakusahau na kuteleza.

Lakini jambo moja nina uhakika nalo kuwa Mashindano hayo hayajaisha. Kwa hakika ndio kwanza yameanza. Wewe unadhani ile Ardhi ya Maradona na sasa Messi kuna anayepata lepe la usingizi? Wanalisubiri kwa hamu na gamu Kombe hilo. Hivyo tukisema Mashindano hayo bado tunayo hatuwezi kuwa mbali sana na ukweli.

Hayo yaliyokuwa Mashindano bora, yaliyotayarishwa vizuri kwa utulivu, Burudani ya hali ya juu. Mshituko na Mshangao vilitawala, David kumuumiza Goliati na kwa mara ya kwanza, Mama Afrika kwenda hatua ambaye alikuwa hajawahi kupiga. Bila shaka mashindano hayo hayajaisha na labda hayatakwisha. Huku nyuma yametuachia athari ambazo itakuwa vigumu kufutika. Sasa tumepata wafalme watatu wa Soka wa kudumu – Pele, Maradona na Messi.

Bidii na kujiamini ni siri ya Mafanikio. Wala usiwe na hofu na yule unayepambana naye. Miujiza imewahi kutokea na bado inatokea. Wapo wakina Thomas walioamini kuwa Qatar isiyo na Hisitoria na Mchezo wa Kakumba inawezaje kuendesha Kombe la Dunia? Mafanikio. Utaratibu. Nidhamu. Mipango. Sifa zote hizi njema zinawaacha wakina Thomas vinywa wazi. Eti nchi za Dunia ya tatu haziwezi kitu. Nawaomba wakasome Qatar!. Haya yalikuwa Mashindano bora yalipangika vizuri. Vikadhihilika vipaji vya wachezaji, waamuzi wakadhihirisha umahiri wa hali ya juu na waliohudhuria wakaishi kwa Salama na amani. Watu wa Tamaduni tofauti walikutana Qatar. Wakaishi vizuri kwa kuheshimiana katika kipindi chote cha Mtanange. Kumbe inawezekana watu wa tamaduni tofauti kukaa pamoja ilimradi kuheshimu tamaduni za wengine. Qatar ilishika msimamo wake wa kutoruhusu Pombe. Na watu wakaheshimu hilo. Matokeo yake zile rabsha ambazo hujitokeza mashabiki wakisha onja, Safari hii hazikuwepo. Kuna somo kubwa kwa watayarishaji wa Mashindano haya ambayo kwa dhahiri yanafanya Dunia kuwa Kijiji. Kama Islamu inavyosisitiza siku zote, Pombe ni Mama wa maasi. Bila Mama mtoto hawezi kuzaliwa. Tujichunge sana na Mama huyu wa maasi.

Bila shaka jitihada za Siasa kuwa mbali na Kabumbu, ni jitihada za Mbuni kufukia Kichwa chake kwenye Mchanga. Upandishaji wa Bendela ni nini kama sio Siasa?. Wimbo wa Taifa unapoimbwa ni nini kama sio siasa iliyopevuka? Yapo yaliyokataliwa lakini yapo yaliyoendelea vichwani mwa watu. Plato hakukosea, binadamu ni kiumbe ambaye amezungukwa na kutengenezwa na Siasa. Bila ya kutarajia au kupanga liliibuka swala la Mwafrika ni nani? Swali hili liliwahi kuwasumbua wasoni kina Ante Diop, Ali Muzrui. Hilo pia lilijitokeza katika Kombe la Dunia Qatar 2022. Hivi Mwafrika ni nani? Ni rangi? Ni Jiografia? Au ni kukiri kuwa mapigo ya moyo ni mali ya Afrika? Wakati michuano inaanza Afrika ilikuwa ina wawakilishi kutoka Ghana, Senegali, Tunisia, Kameruni na Moroko. Kasi ilipoongezeka na wawakilishi wetu wakaanza kupukutika, wana Afrika wakabaki wanashabikia Moroko, lakini wengine wakashabikia Ufaransa ambayo inawachezaji wengi wenye asili ya Afrika. Hapa sasa ndipo mahala pa kujieleza. Hivi Mwafrika ni nani? Morocco si weusi kama sisi Lakini unawezaje kuwanyima haki ya kuwa Waafrika. Gamal Abdul Nasser, ambaye alifungua kituo cha Redio kwa ajili ya ukombozi wa Waafrika, Mkutano wa pili wa Umoja wa Afrika ulifanyika Cairo na mwenyeji alikuwa Gamal Abdul Nasser. Unawezaje kumyima haki ya kuwa Mwafrika? Muamar Ghadaf unamtoaje Afrika, Ahmad Ben Bella aliyewapa mafunzo ya kijeshi wapigania Uhuru, unawezaje kukataa Uafrika wake.

Ukweli ambao hatakama ni mchungu kiasi gani, ni kwamba wale watu weusi katika nchi ya Ufaransa ni Wafaransa na roho zao zinadunda unapoimbwa wimbo wa Taifa lao La Marseillaise. Na ikumbukwe wamekuwa Wafaransa kwa kuchagua na uhuru wa kuchagua ni kanuni ya msingi ya dhana ya Demokrasia. Jambo la kujiuliza kwa nini wamekimbilia Ughaibuni? Mama Afrika anauwezo wa kuwanyonyesha ama anataka wabaki wafe kwa utapiamlo?.

Wakati umefika kwa wana wa Afrika kukomaa. Tukubali na tujielimishe juu ya Historia yetu. Zamani tulipelekwa kwa nguvu ulaya hivi leo hata kwa kuhatarisha maisha yetu tunakimbilia huku. Ni aibu na fedheha. Tunakimbilia ulaya. Kuna kitu Wanahistoria tusaidieni. Ukweli Mwingine ni kuwa watu Weusi popote tulipo tujivunie kwamba hao walitoka kwetu kwenda Ugaibuni, hata wafanyeje, Baraka Obama chimbuko lake ni Kisumu, Kenya na wakati huo huoni Mmarekani kindakindaki. Rangi haiwezi ikawa kigezo cha kuwa mwafrika,Tumepata somo hilo kutoka Qatar.

Miongozo muhimu kwa Wabashiri nchini

Na. Maulana Sheikh Mussa Bin Issa
Mtwara

.....Kutoka toleo lililopita

kisha baada ya ukaguzi tukaanza kuelekea ukumbini na askari kanzu ambaye alikuwa akituongoza alitupa maelekezo kuwa hakuna kupiga makofi wana kushabikia, tutakapotajwa tutasimama na kupunga mikono na kuinama, ukinyanyuka kwenda popote inabidi uiname ndipo uanze kutembea vivyo hivyo utakaporudi. Baada ya malekezo tukaongozwa kuingia- Alhamdulillah ni sauti ya moyoni ambayo itoka kwa muumini baada ya safari hii ndefu au ya kwanza ya kuandika historia katika nchi yetu. tuiingia katika ukumbi No.1 ambapo kwa mbele unamuana vyema Spika wa Bunge. Kila mmoja alikuwa na hisia na hali yake tofauti lakini sawa na nilivyokuwa nawaangaliwa Wazee kwa umakini furaha na hali ya shukurani ilionekana kwa kila mmoja, tulipata fursa ya kuangalia na kujifunza mambo mengi katika Bunge, Maulana Abid Mahmood Bhutt akaniambia huku akicheka kwamba 'Umekumbuka Shura?' sikumjibu ila nikakumbuka maneno ya Khalifat ul Masih II moyoni kwamba Shura yetu itakuwa bora kuliko mabunge makubwa ya ulaya. Baada ya kupita mda na uchangamfu na ukawaida uliporudi moyoni wakati wabunge walipokuwa wanaendelea kutoa michango yao katika uwasilishaji wa marekebisho ya sheria ndogo ndipo Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Mussa Azzan Zungu alitambulisha ujumbe wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya akisema:

"Wageni waliopo Bungeni Mda huu, Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya Mafunzo wageni watano kutoka Jumuiya ya Ahmadiyya Muslim Jamat Tanzania wakiongozwa na Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry ambaye ni Amiri na Mbashiri Mkuu, Karibuni Dodoma, Karibuni Bungeni – Ahsanteni Kwa kuja"

Historia na hatua mpya ya Jumuiya iliandikwa namna hio kwa muujiza na msaada wa Mwenyezi Mungu, baada ya mda tulifuata taratibu za kutoka tukapewa maelekezo na tukatoka nje ya ukumbi, na kupiga picha za kumbukumbu mbele ya Bungu na baada ya hapo tukarejea Makao Makuu ya Mkoa.

Moyo wangu ulikuwa umesharidhika tayari hata sitamani kingine chochote kwani hatua Allah aliyotusaidia niliona inatosha, baada ya sala ya adhuhuri na asir zilizosaliwa kwa pamoja tulikuwa na safari nyingine Muhimu ya kwenda kuonana na Mhe. Joyce L. Ndalichako Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na wenye ulemavu) na muda ulishapangwa na ahadi naye ilisha wekwa, safari ilianza kuelekea katika mji mwingine wa serekali uliopo Msalato, ofisi mpya za majengo ya ghorofa na yaliyokaribu na reli ya kisasa ya mwendo kasi, ni mazingira mazuri sana na ya kuvutia. Tulikaribishwa na kuelekea mpaka ghorofa ya nne kukutana na Mhe. Waziri ambaye alitukaribisha kwa furaha sana. Utambulisho wa jumuiya uliwasilishwa mbele yake na Sheikh Abdur Rahmaan Ame na kisha baada ya hapo Amiri na Mbashiri Mkuu alimpa pongezi kwa uchapa kazi wake na pia kwa ushirikiano tunaopata kama Jumuiya tunapohitaji huduma kutoka katika wizara yake.

Mlango wa mazungumzo ulifungukuka zaidi kwani Mhe. Waziri si mara yake ya kwanza kukutana na Ujumbe wa Jumuiya hivyo anauelewa juu ya jumuiya na kazi zake, ndipo sheikh Abid Mahmood Bhutt Naibu Amiri alinionyesha picha ya ziara ya Mhe. Waziri alipoenda London na Kukutana na Lord Ahmad Tariq ambaye ni mwanajumuiya makini na pia ni mwanasiasa na waziri katika nchi hio, Naibu Amiri alienda kumuonyesha na kumueleza kuwa huyo aliyekutana naye ni MuAhmadiyya pia, alifurahi sana na akajihisi kuwa yupo na ndugu zake bali alimuambia katibu wake kuchukua pia ile na kuitunza. Maulana Khawajah Muzaffar sahib Mbashiri wa Mkoa wa Dodoma alimshukuru Mhe Waziri kwa Unyenyekevu aliotuonyesha na kumuambia kuwa hali hio tumekutana nayo katika ofisi zote za mawaziri tulimopita. Mhe. Waziri Ndalichako aliomba sana sisi kama watumishi wa dini tumuombee sana ili awezi kutimiza majukumu ya kutumikia. Amiri na Mbashiri Mkuu alitoa salamu za shukurani kwake na kwa kutupa fursa ya kujumuika nasi na alichukua fursa hio kumualika katika Jalsa yetu ya mwaka huu, lakini alipoangalia ratiba alisema kuwa siku hizo atakuwepo Kigoma katika jimbo lake ili kuupokea mwenge wa uhuru. Ikasemwa kuwa kama hataweza kuhudhuria basi aandike ujumbe ambao utasomwa mbele za washiriki wa Jalsa.

Alipatiwa nakala ya Qurani tukufu na vitabu vingine vya Jumuiya na kupata picha za pamoja na maombi ya kimya yaliongozwa na Amir na Mbashiri Mkuu na kufunga kikao rasmi na ziara ya siku tatu yenye mafanikio katika historia ya Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya Tanzania ndani ya Jiji la Dodoma. Alhamdulillah.

.....Mwisho

Sharti na Adabu za Kukubaliwa Dua

Kutoka Uk. 12

manabii walikuwa nayo kwa ajili ya maombi hayo. Kwa nini Mtukufu Mtume (saw) alilazimika kufanya maombi kama hayo? Siku zote alikuwa kwenye njia sahihi. Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema kwamba Mitume wangeweza kuomba dua hii ili kupata daraja la juu zaidi. Kwa hakika, Muumini ataomba dua hii huko akhera pia; kama vile hakuna mipaka kwa Mwenyezi Mungu, hakuna mipaka kwa maendeleo ambayo muumini anaweza kuyafanya.

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba hizi ni kanuni na adabu za maombi ambazo zinapaswa kuzingatiwa wakati wa kuomba. Ikiwa watu watafanya hivi, basi wanaweza kupata uzoefu wa ukaribu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu na kujifunza jinsi ya kuomba mahitaji yao mbele Yake.

Kuhusu maombi na adabu zake, Khalifa mtukufu (atba) anamnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye anaeleza zaidi kwamba maombi ni kitu cha ajabu. Hata hivyo, inasikitisha kwamba wanaoomba maombi na wanaoswali katika zama hizi hawajui njia za kupata kupokelewa kwa maombi. Kwa kweli, wako mbali na falsafa ya maombi. Wengine huyakataa maombi tangu mwanzo, na wengine hujitenga na maombi kwa sababu wameghafilika na mbinu za kukubaliwa maombi yao. Watu kama hao wamewapeleka wengine kwenye kuukana uwepo wa Mungu. Kwa ajili ya maombi yenye mafanikio, mtu anapaswa kuwa na subira na uthabiti na asifikirie vibaya juu ya Mungu. Mara nyingi inaonekana kwamba mwombaji anapokaribia kufikia lengo la maombi yake, huchoka na kukata tamaa. Kwa sababu hiyo, wanakataa maombi na hatimaye kukana imani yao juu ya Mungu. Wanadai kwamba ikiwa Mungu kweli angekuwepo, basi bila shaka Angekubali maombi mengi waliyoomba. Watu kama hao wanapaswa kutafakari juu ya ukosefu wao wa imani na subira, kwa sababu hiyo ndiyo sababu ya kweli ya kushindwa kwao. Mtu lazima asiwe na haraka na ajitahidi kuiimarisha imani yake.

Ni Lazima Mtu Avumilie na Asifanye Haraka katika Maombi

Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema kwamba mtu hatakiwi kuchoka. Kisa cha mwombaji ni sawa na mkulima anayepanda mbegu ardhini. Anapanda mbegu inayoweza kuliwa kabisa ardhini, lakini hakuna anayeweza kuelewa kwamba mbegu hiyo sasa inachukua umbo la mmea unaokua. Ndani ya siku chache, mbegu hiyo huanza kuchipua. Tangu wakati mbegu hiyo ilipopandwa ardhini, ilianza maandalizi yake ya kuwa mmea. Mtoto asiye na uzoefu angejiuliza kwa nini mbegu haiwi mmea na kutoa matunda mara moja. Kwa upande mwingine, mkulima, kupitia uzoefu wake, anajua kwamba mchakato huu unahitaji muda. Utaratibu huo huo unahitajika kwa maombi. Maombi yanahitaji lishe, lakini wale wanaofanya haraka kamwe hawaoni matunda ya maombi yao.

Kuhusiana na subira ya muombaji wa kweli, Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema kwamba watu wengi hawashuhudii kamwe matokeo ya maombi yao kwa sababu hawajui hatua za maombi ambazo lazima zivukwe. Wanakuwa na haraka na hawana subira. Mwenyezi Mungu hufanya kazi hatua kwa hatua. Haijawahi kutokea mtu kuoa leo na kupata mtoto siku inayofuata. Ingawa Mungu Yu Mweza wa yote na ni Mwenye Nguvu Zote, hata hivyo ameweka sheria za kutawala ulimwengu.

Kila mtu anafahamu hatua nyingi zinazopaswa kuchukuliwa ili kupata mtoto, nyingi zikiwa ngumu na za hatari. Hadi miezi minne ya ujauzito, hakuna uhakika. Madaktari (kulingana na teknolojia ya wakati huo) waliweza kuchukua skana baada ya wiki 12.

Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema zaidi kwamba mara mtoto anapozaliwa, mama pia huzaliwa upya. Mama huvumilia uchungu mwingi kumzaa mtoto, na baada ya kuzaa kwa uchungu na shida ndipo anapata furaha kwa mtoto wake. Vivyo hivyo katika maombi ni lazima mtu avumilie na kuwa na subira na asiwe mwepesi wa kuchoka. Baada ya kudumu, mtu atashuhudia matokeo ya maombi yake.

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba ni baada ya kujitathmini tu ndipo mtu anaweza kukubaliana na iwapo ameomba kwa bidii au la.

Masihi Aliyeahidiwa (as) anaendelea kusema kwamba mtu lazima aendelee kuomba kwa muda mrefu, kisha ndipo Mwenyezi Mungu Mtukufu atamdhihirikia.

Imeonwa kwamba mwombaji anapobaki kwa kudumu kwenye mlango wa mtu fulani, anapoendelea kuomba-omba na kuzalisha hisia moyoni, anaweza kumuathiri hata mtu mbaya zaidi. Je, mwombaji (kwa Mungu) hapaswi kuwa na bidii kama vile ombaomba (kwa watu)? Mwenyezi Mungu hawezi kamwe kumkataa muombaji ambaye anadumu kumlilia.

Mtu mwenye pupa siku zote huwa katika hasara, na wengine hata wanakuwa makafiri kwa sababu hiyo. Hakuna nguvu zaidi ya Mwenyezi Mungu. Aliwafanya Waarabu kuwa wafalme wa dunia, ambapo kabla hawakuwa chochote. Ikiwa mtu atajitoa kikamilifu kwa Mungu, basi anaweza kupata chochote duniani.

Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema zaidi kwamba ilikuwa ni uaminifu na unyofu wa Ibrahimu (as) uliompa hadhi ambayo aliipata. Aliomba kwamba nabii mkuu atokee miongoni mwa kizazi chake huko Uarabuni. Hakuna aliyeweza kusema jinsi ambavyo dua hiyo ingedhihirika, lakini ilitimizwa kwa utukufu kwa namna ya ujio wa Mtukufu Mtume (saw).

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba kwa kuzingatia mwongozo huu, mtu asiombe tu wakati wa shida bali pia katika nyakati za raha na faraja.

Kiunganishi cha Mwili na Nafsi Kuhusiana na Maombi

Kisha, Khalifa mtukufu (atba) akamnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as), ambaye alieleza kwamba maombi yanahitaji kiunganishi kati ya mwili na roho. Anasema kwamba ikiwa sala na aina nyingine za ibada kama saumu hazina ikhlasi na uaminifu, basi hazina maana yoyote. Masufii na watawa wengi hufanya mila nyingi ambazo huwaletea maumivu, hata hivyo hakuna matokeo. Wanafanya mazoezi ya mwili na mila ambazo hazina athari kwa roho zao. Kwa ajili hiyo, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema katika Qur›ani Tukufu:

Nyama zao hazimfikii Mwenyezi Mungu, wala damu zao, lakini taqwa yenu ndiyo inayomfikia. (Qur'ani Tukufu, 22:38)

Kwa hakika, Mwenyezi Mungu Mtukufu hafurahishwi na ganda tupu, bali Anataka kiini. Maombi lazima yasiwe matupu, badala yake lazima yawe ni maombi ya kweli ya roho. Masihi Aliyeahidiwa (as) anaendelea kusema kwamba sasa swali linazuka, kuna haja gani ya kusali wakati ni roho tu iliyo nyuma yake ndiyo inayomfikia Mungu? Mtu angeweza tu kusali katika moyo wake kwa unyofu na kusingekuwa na haja ya matendo ya kiibada. Jibu kwa hili ni kwamba wale wanaoacha vitendo vya kimwili hawawezi kuiathiri nafsi na roho zao. Kwa upande mwingine, ikiwa mtu anatumia tu mwili na njia zake za kimwili, huyo pia amekosea sana. Mwili na roho vimeunganishwa; ikiwa mtu analia hata kwa njia isiyo ya kweli, mwishowe atakuwa na hisia za kweli, na ikiwa mtu atatabasamu kwa uwongo, mwishowe atakuwa na kicheko. Sawa na hali ya maombi. Ikiwa mwili unaonyesha unyenyekevu, sala pia itabeba roho hiyo hiyo. Kusujudu kutupu ni ubatili isipokuwa kuambatane na unyenyekevu wa kweli. Ni kwa sababu hii kwamba sijda ndio kilele cha sala. Wanyama huonyesha hali hii pia.

Khalifa mtukufu (atba) anasema kwamba mwili pia hudhihirisha kile kinachohisiwa na roho. Ikiwa roho ina dhiki, basi mwili pia unaonyesha dalili za uchovu na kuelemewa.

Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema zaidi kwamba ulimwengu wa kimwili na wa kiroho hufuatana. Kwa hiyo, ni muhimu kwamba wakati wa kuomba, mtu aonyeshe unyenyekevu wake kupitia matendo yake. Hata ikiwa mwanzoni ni kuigiza tu, lakini polepole hukua kuwa kitu cha dhati. Matokeo yake, mtu hatamwendea Mungu Mwenyezi katika wakati wa uhitaji tu, bali atabaki kwenye kizingiti cha Mungu kila wakati.

Kujinyima Faraja Ili Kupata Furaha Katika Maombi

Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema zaidi furaha na faraja huja baada ya maumivu. Ni kwa sababu hii kwamba Quran Tukufu inasema:

Hakika upo wepesi baada ya dhiki. (Qur'ani Tukufu, 94:7)

Kwa hivyo, ikiwa mtu hapati raha katika Sala, anapaswa kutathmini kama amevumilia shida na maumivu kwa ajili ya Sala yake. Mtu anapaswa kuzingatia masharti yote ya maombi na kuyatekeleza kwa wakati. Zaidi ya hayo, mtu anapaswa kujitolea usingizi wake kwa ajili ya Sala.

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba wakati mwingine, watu hawaweki juhudi katika maombi yao wenyewe na wanafikiri kwamba matatizo yao yatatatuliwa ikiwa watawaomba wengine wawaombee. Watu kama hao hawasali hata sala zao tano za kila siku mara kwa mara. Katika suala hili, kijana mmoja alimwomba Masihi Aliyeahidiwa (as) amwombee baba yake. Kwa kujibu, Masihi Aliyeahidiwa (as) alishauri kwamba anapaswa kuomba kwa bidii yeye mwenyewe. Iwapo angeomba yeye mwenyewe, ni hapo tu ndipo maombi ya Masihi Aliyeahidiwa (as) yangekuwa na manufaa kwake.

Masihi Aliyeahidiwa (as) anaendelea kusema kwamba mtu anapojitwika maumivu na kuacha mambo yanayomchukiza Mungu, basi mtu kama huyo ataweza kuipatia nafsi yake athari njema. Matatizo kama haya yanayovumiliwa kwa ajili ya Mungu yataathiri nafsi, na hii itaifanya nafsi kumwomba Mungu kikweli. Watu wengine hucheza ala au kuzunguka huku na huku kama ibada. Ingawa vitu hivi ni vya kufurahisha, havina athari kwa roho. Mataifa mengine hayajali jambo hili kwa sababu hawajaelewa falsafa ya kweli ya sala.

Zaidi ya hayo, Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema kwamba Ibrahimu alikuwa mwaminifu na mnyofu kwa Mungu, hivyo alitunzwa cheo cha juu. Unyofu kwa Mungu unahitaji aina fulani ya kifo, na ni baada tu ya kukubali kifo hicho ndipo mtu anaweza kuwekwa wakfu kwa Mungu. Ibada ya masanamu haikomei tu kuabudu mti au jiwe, badala yake, chochote kinachotuzuia tusipate upendo wa Mungu huongoza kwenye ibada ya masanamu. Kila mtu ametengeneza sanamu ndani yake, na ni pale tu mtu anapoacha kila kitu kwa ajili ya Mungu ndipo anapoweza kujiweka huru kutokana na ibada ya masanamu.

Ibrahimu (as) alipokubali kumtoa mwanawe kafara kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, basi Mwenyezi Mungu alimlinda na kila aina ya maumivu. Alitupwa kwenye moto lakini haukuweza kumteketeza. Yote haya ni matokeo ya mwili na roho; lazima kuwe na muunganisho, vinginevyo sala zisizo na hii ni bure.

Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema zaidi kwamba kila kitu kina wakati wake. Mtu anayejaribu kufikia kitu kwa wakati usiofaa hakika atashindwa. Wakati wa shida, mtu anapokimbilia kwenye maombi, kwa hakika inawezekana kwamba mitihani zaidi humjia mtu huyo. Kisa cha Musa (as) ni mfano mkuu wa hili. Alipotaka kupunguza mateso ya watu wake, yaliongezeka mara nyingi. Musa (as) aliwausia watu wake wawe na subira, lakini walizidi kuhangaika. Hatimaye, waliamrishwa kuhama. Wakati huo, Farao aliwafuata, na watu wakakata tamaa wakifikiri kwamba wangekamatwa. Hata hivyo, Musa (as) alikuwa na imani kwamba Mungu wake alikuwa pamoja naye. Walilazimishwa kuvuka mto Nile salama, na Farao akakabili mwisho wake. Hii ndiyo njia ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu huwasaidia wale wanaomuomba kwa ukweli. Hata hivyo, kabla ya msaada huo kuonekana, mtu hupatwa na majaribu ambayo nyakati fulani huonekana kuwa hayawezi kuvumilika.

Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema kwamba mtu anatakiwa kuwa mnyenyekevu na kumuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa uchungu na kutotulia. Kwa hakika, kuomba kwa maumivu na hisia ni ishara kwamba maombi ya mtu yatakubaliwa. Hivyo, mtu hapaswi kumfikiria Mungu vibaya na kuanguka katika hali ya kukata tamaa. Bali, mtu anapaswa kujaribu kusali na kuomba kwa uchungu na unyenyekevu hasa katika nyakati za raha na faraja, badala ya nyakati za shida tu.

Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema kwamba muumini anapaswa kuwa imara kila wakati na asianguke kwenye mawindo ya uvivu. Mtu anapaswa kuwa na shauku ya kufanya matendo mema na kusonga mbele zaidi katika wema.

Mwishowe, Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba tunapaswa kuwaombea Waahmadiyya walioko Pakistan na katika sehemu nyinginezo za dunia kama vile Algeria ambao wanakabiliwa na ukatili na ubaguzi. Khalifa mtukufu (atba) aliomba kwamba Mwenyezi Mungu awalinde Waahmadiyya kote duniani na kubatilisha mashambulizi na juhudi za maadui.

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

Mapenzi ya Mungu

AKHIRA - RAJAB. 1444 AH | JANUARI 2023 | ZAHOOR 1402 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufusaw

Abu Huraira^ra anasimulia kwamba: Nilimsikia Mtume^saw akisema: Abu Huraira wallahi mimi naomba msamaha kwa Allah kutubia kwake kwa siku moja zaidi ya mara sabini (**Bukhari**).

Sharti na Adabu za Kukubaliwa Dua

Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa Ukarimu

Kanuni za Maombi na Haja ya Unyenyekevu na Uthabiti.

Baada ya kusoma *Tashahhud*, *Ta›awwuz* na *Surah al-Fatihah*, Khalifa mtukufu, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (aba) alisema kwamba watu wengi huuliza kuhusu maombi. Hasa zama hizi, watu wengi wanahoji kuhusu maombi na kumhusu Mungu. Kwa kweli, inaonekana kwamba kuna mashambulizi yaliyopangwa dhidi ya Mungu na watu wasioamini juu ya uwepo wa Mungu. Watu wanapelekwa mbali na Mungu. Katika hali kama hizi, hata watu wetu wanakuwa mawindo wa mawazo kama hayo ya kishetani na kuwafanya wawe na mashaka kuhusu maombi, Mungu, na imani yao pia.

Mashaka Kuhusu Swala (Maombi)

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba katika kukabiliana na mtihani au kushindwa, wale ambao ni dhaifu wa imani au walio na uelewa mdogo hufikiri kwamba imani yao ni ya uongo na hakuna ukweli juu yake au kwamba Mungu hatawarehemu na kuwaokoa kutoka kwenye matatizo yao. Wanahisi kwamba Mungu ni mkatili kwao kutokana na hali zao. Wanahisi kwamba licha ya kuomba, hali zao hazibadiliki.

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba maswali na mashaka hayo yanatokea katika akili za wale ambao wana mwelekeo zaidi wa kidunia. Wengi wa watu kama hao wanamwandikia Khalifa mtukufu (atba) pia, wakieleza maoni yao mabaya. Badala yake, mtu anapaswa kujitafakari na kutathmini jinsi anavyotimiza haki za Mungu, na kiwango cha ibada yake ni kipi.

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba leo, atazungumzia kuhusu maombi na falsafa yake, adabu zake, wajibu wetu, haja ya maombi na ulazima wa kuwa na imani thabiti kwa Mungu kwa kupitia maandishi ya Masihi Aliyeahidiwa (as).

Maombi Lazima Yafanyike Wakati wa Faraja na Dhiki

Khalifa mtukufu (atba) amemnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba ni kutokana na rehema za Mwenyezi Mungu tu kwamba mtu anawezeshwa kuwa na hofu wakati wa faraja kama vile anavyoogopa wakati wa dhiki. Asiyemsahau Mwenyezi Mungu wakati wa raha hatasahauliwa na Mwenyezi Mungu wakati wa magumu. Hata hivyo, wale wanaotumia wakati wao wa faraja katika starehe na wakakimbilia tu kuswali wakati wa shida, maombi yao hayakubaliwi. Inapokuja adhabu ya Mwenyezi Mungu, basi milango ya kukubaliwa maombi hufungwa.

Hakika wachamungu ni wale wanaodumu katika hali ya maombi kabla haijawajia adhabu kama hiyo, wanakuwa ni wenye kutoa mali zao, na kutekeleza amri za Mwenyezi Mungu na ni wema kwa viumbe vya Mwenyezi Mungu.

Masihi Aliyeahidiwa (as) anaendelea kusema kwamba mti hutambuliwa kwa matunda yake sawa na jinsi mchamungu anavyojipambanua kwa wema wake.



Masjid Mubarak: Hadhrat Ameerul Mumineen Mirza Masroor Ahmad, Khalifatul Masih wa V^atba akihutubia Ijumaa ya Tar. 16.12.2022.

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba mtu hatakiwi kumsahau Mungu, na ikiwa mtu anaitimiza haki hii, basi Mwenyezi Mungu Mtukufu humuokoa mtu wa aina hiyo kutoka kwenye shida. Shughuli zetu za kidunia zisituondoe katika kumuabudu na kumwomba Mungu Mwenyezi.

Kumuomba Mungu Kunahitaji Kumuheshimu

Akifafanua zaidi jinsi mtu anavyopaswa kumwomba Mwenyezi Mungu, adabu za maombi na jinsi Mwenyezi Mungu Alivyotupandikizia adabu hizi Yeye Mwenyewe, Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema kwamba kumwomba Mwenyezi Mungu kunataka kumuheshimu. Watu wanapoomba jambo fulani kwa mfalme wao, wanahakikisha kwamba wanamuonyesha heshima. Ni kwa sababu hii kwamba tunazitaja sifa za Mwenyezi Mungu na kumsifu katika *Surah al-Fatihah*.

Tunamwita mwenye kustahili sifa zote, *Rahmaan* (Mwenye rehema) na *Rahiim* (Mwenye kurehemu). *Rahiim* ina maana kwamba haruhusu juhudi za kweli kupotea. Zaidi ya hayo, tunamwita Mwenyezi Mungu Mtukufu kama Bwana wa Siku ya Hukumu, kwani Yeye ndiye Hakimu siku hiyo.

Mara tunapomtambua Mungu Mwenyezi kuwa yuko, basi tunamsihi atuonyeshe njia iliyo sawa; njia iliyonyooka. Kuna njia ambayo watu huikanyaga, lakini juhudi zao zinapotea bure. Kwa upande mwingine, kuna njia nyingine ambayo juu yake juhudi zote za mtu binafsi huzawadiwa. Baada ya hapo, tunaomba kuongozwa kwenye njia ya waliokubaliwa. Zaidi ya hayo, tunaomba ulinzi kutokana na njia ya wale ambao wamemkasirisha Mwenyezi Mungu na wakapotea.

Masihi Aliyeahidiwa (as) anasema zaidi kwamba tunapoomba mwongozo wa njia sahihi, inajumuisha njia zote za kidunia na za kiroho. Kwa mfano, daktari hawezi kumtibu mgonjwa bila kukanyaga njia sahihi. Vile vile taaluma na mafanikio yote yanamhitaji mtu kukanyaga njia sahihi, na hili linaweza kupatikana tu ikiwa mtu ana uhusiano na Mwenyezi Mungu.

Adabu za Maombi

Wakati Masihi Aliyeahidiwa (as) alipokuwa akisema hivi, mtu mmoja katika hadhara aliuliza ni haja gani

Endelea uk. 11



Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad, Masihi Aliyeahidiwa na Mahdi^as aliandika Qaseedah ya Karabu (Lyric Shairi) katika kitabu chake ***A'ina'-e-Kamalaat-e-Islam***, akielezea mapenzi yake kwa Mtukufu Mtume Muhammad^saw. Kasidah ni Tafsiri ya Kiswahili ya shairi hili Kuhusu Qaseedah Masihi Aliyeahidiwa^as aliandika: Hii ni Qaseedah ya ajabu na nzuri iliyojaa fasihi uzuri na johari nzuri za lugha ya Kiarabu, na imeandikwa kwa kumsifu bwana wangu na kiongozi wa walimwengu wote wawili, Hazrat Khaatam-un-Nabiyyeen Muhammad^saw. Kuandika hii Qaseedah ilikuwa haiwezekani kwa sababu ya asili yangu dhaifu na ya unyenyekevu—chochote nitakacho wamesema imetoka kwa Mwenyezi Mungu. Ubora wa fasihi, ya kuvutia mazungumzo, na maneno ya kuvutia na ya kina ambayo kwayo unaona upekee na unadra sio bidhaa yangu mwenyewe juhudi; lakini hata hivyo Mwenyezi Mungu amenipa ukuu juu ya haya waandishi walio hodari wa kalamu, na hii ni Ishara kutoka kwa Mola wangu kuwaendea wenye Elimu. Nimeeleza jambo hili kwa kusudi pekee nipate thawabu kwa kushukuru, na ili nisihesabiwe miongoni mwa wasio shukuru. Masihi Aliyeahidiwa inaripotiwa kuwa alisema: 'Hii Qaseedah imekubaliwa na Allahu, na Allah amenijulisha kwamba yeyote yule atakayehifadhi Qaseedah hii na kuirudia mara kwa mara, moyo wa mtu kama huyo atapewa mapenzi mazito Kwangu Mimi na kwa Mtume Muhammad^saw na Nitamlipa kwa ukaribu Wangu.

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com